Taarifa kwa Vyombo vya Habari
Katazo: Jumatatu 25 Januari 2021

Linapatikana pia katika Kiarabu, Kifaransa na Kiswahili

Vitabu vya Watoto vya Kiafrika kuhusu uendelevu na usawa kuangaziwa katika chama kipya cha vitabu cha Malengo ya Maendeleo Endelevu

Hatua mpya ya wingilugha imeleta pamoja mashirika ya sekta ya vitabu kutoka kote barani Afrika ili kujitolea katika kukuza Chama cha Vitabu cha Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa kwa kutoa mchango wa vitabu vya watoto vinavyohusu Malengo ya Maendeleo Endelevu mbalimbali katika lugha za Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu na Kiswahili.

Chama hiki cha vitabu kitazinduliwa mnamo Siku ya Vitabu Duniani (tarehe 23 Aprili 2021). Uzinduzi huu utaangazia vitabu bora vinavyoshughulikia maudhui ya Malengo ya Maendeleo Endelevu. Mawasilisho ya vitabu husika yanapokelewa kwa sasa kupitia http://bit.ly/SDGBookClubAfrica na kamati ya uteuzi iliyoundwa na wambia mbalimbali. Kamati hiyo itateua orodha teule ya vitabu katika kila Lengo la Maendeleo Endelevu.

Samuel Kolawole, Mwenyekiti wa Mtandao wa Wachapishaji wa Kiafrika (*APNET*) alisema: Bila shaka vitabu bora vya viwango vyote vinaweza kuchangia pakubwa katika kufikiwa kwa Malengo ya Maendeleo Endelevu ulimwenguni kote kupitia kutoa maarifa kuhusu malengo hayo na hatua zinazoweza kuchukuliwa ili kuyafikia. Kwa Afrika, kuwepo na kupatikana kwa vitabu kama hivyo ambavyo vimechapishwa kiasilia Afrika na ambavyo Waafrika wanaweza kujihusisha navyo, kutasaidia sana katika kuhakikisha kuwa bara la Afrika linapiga hatua nzuri katika kuyafikia Malengo ya Maendeleo Endelevu. Hii ndiyo sababu kwamba juhudi za washikadau wote katika sekta ya vitabu barani kote, kwa kushirikiana na Umoja wa Mataifa, za kuunda Chama cha Vitabu cha Malengo ya Maendeleo Endelevu Afrika zinahitaji kupongezwa na kuungwa mkono na watu wote.

Olatoun Gabi-Williams, Mwanzilishi wa *Borders Literature for all Nations* alisema: Ni jambo zuri sana kujua kwamba vitabu vya watoto vilivyochapishiwa Afrika, vikiwa na jumbe zito kuhusu Malengo ya Maendeleo Endelevu, vitakuwa sehemu muhimu ya mkusanyiko wa vitabu vya watoto ulimwenguni kupitia jukwaa hili – Chama cha Vitabu cha Malengo ya Maendeleo Endelevu Tawi la Afrika.

Lily Nyariki, Shirika la Maendeleo ya Elimu Afrika (*ADEA*) alisema: Hii ni hatua faafu ambayo itaiwezesha Afrika kuchangia maarifa ya ulimwengu kupitia vitabu vya watoto huku ikiwaangazia wachapishaji na waandishi wa Kiafrika katika jukwaa la kimataifa. *ADEA* inawahongera waandishi na wachapishaji wanaoshiriki.

Bw. Mandla Ntombela, Rais wa Maktaba za Kiafrika na Mashirika ya Habari na Taasisi (*AFLIA*) aliongezea: Maktaba za Kiafrika na Mashirika ya Habari na Taasisi (*AFLIA*) yanaunga mkono kikamilifu Tawi la Afrika la Chama cha Vitabu cha Malengo ya Maendeleo Endelevu kwa kuwa hakuna mlingano wa thamani ya habari ama kupitia vitabu vya hadithi au vitabu vya kiada katika kutoa maarifa yanayoweza kuchochea akili kuweza kuwa rasilimali ya kutatulia matatizo ya kijamii. Kuimarisha njia na uwezekano wa kufikiwa kwa Malengo ya Maendeleo

Endelevu kupitia kusoma ni wazo linalopokewa kwa mikono miwili katika maktaba za Kiafrika.

Dkt. Wale Okediran, Katibu Mkuu, Shirika la Waandishi Wote wa Kiafrika (*PAWA*) alisema: *PAWA* inafurahia kuwa sehemu ya mradi huu wa ajabu ambao kupitia kwao watoto wa Kiafrika wanaweza kujihusisha na jumbe za Malengo ya Maendeleo Endelevu katika muktadha wa mazingira yao kupitia vitabu vilivyoandikwa na kuchapishwa na Waafrika.

Mr. Dare Oluwatuyi, Rais wa Shirika la Wauzavitabu Naijeria (*BAN*) aliongezea: Tunafurahia kuwa sehemu ya mradi huu wa Chama cha Vitabu cha Malengo ya Maendeleo Endelevu ambao, kwa maoni yetu, utafanikisha mambo mawili, pamoja na mengineyo, ushindi. Jambo la kwanza ni msisitizo mkubwa juu ya utamaduni wa kusoma na kuandika barani Afrika na la pili, mawasiliano yenye athari kubwa mashinani kuhusu malengo sifika - Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa. Sisi, vilevile, tunawahimiza wengine kuunga mkono mradi huu.

Anthea Basson, Ofisa wa Kitaifa wa Habari, *UNIC* (Kitovu cha Habari cha Umoja wa Mataifa) Windhoek: Chama cha Vitabu cha Malengo ya Maendeleo Endelevu Tawi la Afrika kinafungua shabaha kuu za Malengo ya Maendeleo Endelevu kupitia hadithi ambazo zinaweza kuwatia moyo watoto. Simulizi katika kitabu cha watoto ni nafasi nzuri ya kufundishia na kutolea mifano inayohusu Malengo ya Maendeleo Endelevu na umuhimu wa kuchukua hatua zifaazo. Kusoma ni stadi ya kimsingi ambayo inakuza stadi nyingine nyingi. Je, ni njia ipi nyingineyo mwafaka ya kutalii Malengo ya Maendeleo Endelevu iliyo bora kuliko kitabu?

Chama cha Vitabu cha Malengo ya Maendeleo Endelevu cha Kiafrika kinafuatia uzinduzi wa vyama wa hivi karibuni katika mataifa ya Norwe, Indonesia, Ureno na Brazili. Jumuia ya uchapishaji ulimwenguni kupitia Chama cha Kimataifa cha Wachapishaji (IPA) inaunga mkono Malengo ya Maendeleo Endelevu kama namna ya kuwekeza katika vizazi vijavyo vya viongozi, wavumbuzi na mawakala wa mabadiliko.

Wambia waanzilishi wa Tawi la Afrika la chama hiki cha vitabu ni:

- Pan African Writers' Association (PAWA)
- Pan African Booksellers Association (PABA)
- Association for the Development of Education in Africa (ADEA)
- African Publishers Network (APNET)
- African Library & Information Associations & Institutions (AfLIA)
- Borders Literature for all Nations
- United Nations Information Centre Windhoek

Mashirika ambayo yangependa kujiunga na mradi huu yanaalikwa kuwasiliana na:

- **Welda Mouton, UNIC:** mouton@un.org
- **Dr Wale Okediran, PAWA:** waleokediran@yahoo.co.uk

Kuhusu Chama cha Vitabu cha Malengo ya Maendeleo Endelevu

Chama cha Vitabu cha Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa kilizinduliwa jijini Bologna wakati wa Maonyesho ya Kimataifa ya Vitabu vya Watoto ya mwaka wa 2019. Chama hiki hudhamiria kutumia vitabu kama kifaa cha kuwatia moyo watoto wa umri wa miaka 6-12 ili kutagusana na misimamo ya Malengo ya maendeleo endelevu (SDGs) kupitia vitabu vya kusomwa kutoka kote ulimwenguni vinavyohusiana na kila mojawapo ya malengo 17 katika lugha zote sita rasmi za Umoja wa Mataifa – Kiarabu, Kichina, Kiingereza, Kifaransa, Kirusi na Kihispania.

https://www.un.org/sustainabledevelopment/sdgbookclub/

Kuhusu Malengo ya Maendeleo Endelevu

Malengo 17 ya Maendeleo Endelevu yalipitishwa na viongozi kutoka kote ulimwenguni wakati wa Mkutano wa kihistoria wa Maendeleo Endelevu mnamo Septemba 2015. Kupitia kushughulikia masuala yote kutoka afya, hadi usawa wa kijinsia na elimu, Malengo haya yatahamasisha jitihada kutoka ulimwenguni kote ili kuangamiza aina zote za umaskini, kupambana na hali zinazozuia usawa na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, huku ikihakikishwa kwamba hakuna yeyote anayebaki nyuma.

https://www.un.org/sustainabledevelopment/